# TUJIFUNZE BIBLIA

## *SOMO LA 9*

### ROHO MTAKATIFU NA MIUJIZA

Watu wengi wa siku zetu wanasumbuliwa sana kwa habari ya Roho Mtakatifu. Wanataka kujua kwamba ni nani awezaye kupewa Roho, kwamba watu wanampokea Roho kwa njia gani, na kwamba Roho anafanya kazi gani siku hizi. Katika somo hili, tutajaribu kuyachunguza maneno ya Mungu tupate kuelewa mambo hayo.

Jambo la kwanza, tuone kwamba ni watu gani wanaoweza kumpokea Roho. Safari moja mitume walikuwa wakihubiri habari ya kufa na kufufuka kwake Yesu. Kisha walisema:

"*Na sisi tu mashahidi wa mambo haya, pamoja na Roho Mtakatifu ambaye Mungu amewapa wote wamtiio.*" Matendo 5:32

1. Watu wangapi wanaweza kupata Roho Mtakatifu? __________________
2. Je! watu hupewa Roho Mtakatifu kusudi waweze kumtii Mungu au kwa sababu wamekwisha kumtii? __________________

Siku ya Pentekoste Petro aliwaambia watu jinsi iwapasavyo kumtii Mungu kusudi wapąte Roho.

"*Petro akawaambia, Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.*" Matendo 2:38

3. Watu hupewa Roho wanapomtii Mungu katika kutubu pamoja na kufanya nini? __________________

Baada ya mtu kuamini, kutubu dhambi zake, na kubatizwa katika maji, Roho Mtakatifu humwingia na kukaa naye. Twasoma:

"*Hamjui ya kuwa ninyi mmekuwa hekalu la Mungu, na yakuwa Roho wa Mungu anakaa ndani yenu?... Au hamjui yakuwa mwili wenu ni hekalu la Roho Mtakatifu aliye ndani yenu, mliyepewa na Mungu? Wala ninyi si mali yenu wenyewe.*" 1 Wakorintho 3:16; 6:19

"*Ikiwa Roho wa Mungu anakaa ndani yenu, ninyi hamwufuati mwili; bali mwaifuata roho. Lakini mtu awaye yote asipokuwa na Roho wa Kristo, huyo si wake.*" Warumni 8:9

4. Mwili wa Mkristo ni hekalu la nani? __________________
5. Mtu asipokuwa na Roho wa Kristo atakuwa si mali ya nani? __________________

Mistari ya Biblia tuliyoisoma huko juu imetuonyesha waziwazi kwamba kila Mkristo hupata Roho Mtakatifu anapomtii Mungu akitubu na kubatizwa. Tena, ni lazima kwa mtu kupata Roho, maana asiyepata Roho si mali ya Yesu!

## MIUJIZA NA ISHARA

Katika Marko 16:15-18 twasoma maneno ya Yesu jinsi alivyowaambia mitume akisema:

"*Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe. Aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini, atahukumiwa. Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; kwa jina angu watatoa pepo; watasema kwa lugha mpya; watashika nyoka; hata wakinywa kitu cha kufisha, hakitawadhuru kabisa; wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, nao watapata afya.*"

Watu wengine wameelewa vibaya maneno hayo ya Yesu wakidhani kwamba kila mtu atakayemwamini atapewa uwezo wa kufanya miujiza. Walakini, tangu mwanzo haikuwa mpango wa Mungu kwamba kila Mkristo aweze kufanya ishara au miujiza. La! bali katika siku za mitume kila Mkristo alipewa kazi yake na uwezo wake tofauti na mwenzake. Kwahiyo, baadhi tu ya Wakristo walipewa uwezo wa kufanya miujiza. Tunaweza kuthibitisha jambo hili katika Biblia. Twasoma:

"*Mtu mmoja kwa Roho apewa neno la hekima; na mwingine neno la maarifa, apendavyo Roho yeye yule; mwingine imani katika Roho yeye yule; na mwingine karama za kuponya katika Roho yule mmoja; na mwingine matendo ya miujiza; na mwingine unabii; na mwingine kupambanua roho; mwingine aina za lugha na mwingine tafsiri za lugha; lakini kazi hizi zote huzitenda Roho huyo mmoja, yeye yule, akimgawia kila mtu peke yake kama apendavyo yeye… Je! wote ni mitume? wote ni manabii? wote ni waalimu? <u>wote wanatenda miujiza?</u> <u>wote wana karama za kuponya wagonjwa?</u> <u>wote wanena kwa lugha?</u> wote wafasiri?*"

Wakorintho 12:8-11,29-30

6. Je! katika siku za mitume, Wakristo wote walikuwa manabii? __________________

7. Je! wote waliweza kufanya miujiza? __________________

8. Je! wote waliweza kunena kwa lugha? __________________

Biblia inatuambia habari ya watu ambao hawakufanya miujiza hata ingawa walikuwa wamejawa Roho Mtakatifu. Yohana Mbatizaji ni mmoja wapo kati ya hawa. Ebu! tuone habari zake Yohana katika Biblia. Kabla Yohana hajazaliwa malaika wa Mungu, alimwambia babaye akisema:

"*Usiogope, Zakaria, maana dua yako imesikiwa, na mkeo Elisabeti atakuzalia mtoto mwanamume, na jina lake utamwita Yohana… naye atajazwa Roho Mtakatifu hata tangu tumboni mwa mamaye.*"

Luka 1:13,15

Hata ingawa Yohana alijazwa Roho, lakini twasoma:

"*Na watu wengi wakamwendea* (Yesu)*, wakasema, Yohana kweli hakufanya ishara yo yote, lakini yote aliyoyasema Yohana katika habari zake huyu* (Yesu) *yalikuwa kweli.*" Yohana 10:41

9. Yohana Mbatizaji alijazwa Roho Mtakatifu hata tangu lini? __________________

10. Hata ingawa Yohana alijazwa Roho, walakini hakufanya nini? __________________

## UBATIZO WA ROHO

Kubatizwa katika Roho na kujawa Roho ni mambo mawili tofauti. Kila Mkristo anaweza kujawa Roho bali ahadi ya kubatizwa katika Roho ilitolewa kwa mitume wa Yesu. Mitume walipewa ahadi hii kusudi Roho awasaidie katika kutoa ushuhuda wa kufufuka kwake Yesu. Shahidi ni mtu aliyeona jambo kwa macho yake. Sisi leo si mashahidi wa Yesu kwa sababu hatukumwona alipofufuka. Basi, Yesu aliwaahidi mitume akisema:

"*Lakini ajapo huyo Msaidizi, nitakayewapelekea kutoka kwa Baba, huyo Roho wa kweli atokaye kwa Baba, yeye atanishuhudia. <u>Nanyi pia mnashuhudia, kwa kuwa tangu mwanzo mmekuwapo pamoja nami.</u>*"

Yohana 15:26-27

"*Hata siku ile (Yesu) alipochukuliwa juu, alipokuwa amekwisha kuwaagiza kwa Roho Mtakatifu <u>wale mitume</u> aliowachagua; <u>wale aliowadhihirishia nafsi yake, kwa dalili nyingi baada ya kuteswa kwake, ya kwamba yu hai</u>, akiwatokea muda wa siku arobaini, na kuyanena mambo yaliyouhusu ufalme wa Mungu. Hata alipokuwa amekutana nao aliwaagiza wasitoke Yerusalemu, bali waingoje ahadi ya Baba, ambayo mlisikia habari zake kwangu; ya kwamba Yohana alibatiza kwa maji, bali ninyi mtabatizwa katika Roho Mtakatifu baada ya siku hizi chache… Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; <u>nanyi mtakuwa mashahidi wangu</u> katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi.*"

Matendo 1:2-5,8

11. Mitume walikuwa mashahidi wa Yesu maana walikuwapo pamoja naye tangu lini? _________________

12. Yesu aliwaahidi nani kwamba watabatizwa katika Roho? _________________

13. Yesu aliwaambia mitume kwamba watapata nguvu ya kumshuhudia wakati atakapowajilia nani? _________________

Kwa sababu Yuda Iskariote alijiua kabla Yesu hajafufuka katika wafu, basi Yesu alimchagua Mathiya kuwa mtume na shahidi pamoja na wale kumi na mmoja (Matendo 1:21-26). Siku ya Pentekoste mitume hawa wote walikuwako mahali pamoja. Kisha twasoma:

"*Kukawatokea ndimi zilizogawanyikana, kama ndimi za moto uliowakalia kila mmoja wao. Wote wakajazwa Roho Mtakatifu, wakaanza kusema kwa lugha nyingine, kama Roho alivyowajalia kutamka… Basi sauti hii iliposikiwa makutano walikutanika, wakashikwa na fadhaa, kwa kuwa kila mmoja aliwasikia, wakisema kwa lugha yake mwenyewe. Wakashangaa wote, wakastaajabu wakiambiana, Tazama, hawa wote wasemao si Wagalilaya? Imekuwaje basi sisi kusikia kila mtu lugha yetu tuliyozaliwa nayo?*"

Matendo 2:3-4,6-8

14. Yesu alikuwa na wanafunzi wengi wasiokuwa Wagalilaya bali mitume wote walikuwa Wagalilaya (Matendo 1:10-13). Je! watu wote waliosema kwa lugha siku ya Pentekoste walikuwa Wagalilaya? _________________

15. Basi, watu wale waliobatizwa na Roho siku ya Pentekoste hawakuwa wanafunzi wote bali walikuwa nani? _________________

Mwanafunzi akisoma kwa uangalifu Matendo 2:4,43; 3:3-8; na 4:33 ataona kwamba waliokuwa wakifanya miujiza baada ya siku ya Pentekoste walikuwa mitume. Tena, twasoma:

"*Na kwa mikono ya* <u>*mitume*</u> *zikafanyika ishara na maajabu mengi… na katika wote wengine hapana hata mmoja aliyethubutu kuambatana nao.*" Matendo 5:12-13

16. Kwa sababu ya maajabu na ishara ambazo mitume walikuwa wakizifanya, Wakristo wote wengine hawakuthubutu kufanya nini? _________________

Wakristo walipozidi kuwa wengi sana, mitume waliweka mikono yao juu ya watu wengine saba kusudi waweze kuwatumikia wenzao. Watu hao waliochaguliwa walikuwa wamejawa Roho Mtakatifu kabla hawajawekewa mikono ya mitume. Walakini, hawakufanya ishara kabla ya kuwekewa mikono. Ebu! tuone mambo hayo katika Biblia.

"*Wale Thenashara* (yaani, mitume 12) *wakawaita jamii ya wanafunzi, wakasema, Haipendezi sisi kuliacha neno la Mungu na kuhudumu mezani. Basi ndugu, chagueni watu saba miongoni mwenu, walioshuhudiwa kuwa wema,* <u>*wenye kujawa na Roho*</u>*, na hekima, ili tuwaweke juu ya jambo hili; na, sisi tutadumu katika kuomba na kulihudumia lile Neno. Neno hili likapendeza machoni pa mkutano wote; wakamchagua Stefano, mtu aliyejaa imani na Roho Mtakatifu, na Filipo, na Prokoro, na Nikanori, na Timoni, na Parmena, na Nikolao mwongofu wa Antiokia; ambao wakawaweka mbele ya mitume, na walipokwisha kuomba wakaweka mikono yao juu yao… Na Stefano, akijaa neema na uwezo, alikuwa akifanya maajabu na ishara kubwa katika watu.*" Matendo 6:2-6,8

17. Stefano, Filipo, na wenzao walijawa Roho Mtakatifu kabla hawajawekewa mikono. Walakini, twasikia kwamba Stefano alipata uwezo wa kufanya ishara na maajabu baada ya kuwekewa mikono ya nani? _________________

Baada ya muda kadhaa Wakristo walianza kuteswa huku Yerusalenu. Basi, wote walitawanyika isipokuwa mitume (Matendo 8:1-4). Filipo aliyekuwa mmojawapo wa watu wale saba waliowekewa mikono ya mitume, aliingia mji wa Samaria, akawahubiri Kristo. Kisha twasoma:

"*Na makutano kwa nia moja wakasikiliza maneno yale yaliyosemwa na Filipo walipoyasikia na kuziona ishara alizokuwa akizifanya… Lakini walipomwamini Filipo, akizihubiri habari njema za ufalme wa Mungu, na jina lake Yesu Kristo, wakabatizwa, Wanaume na wanawake… Na mitume waliokuwako Yerusalermu, waliposikia ya kwamba Samaria imelikubali neno la Mungu, wakawapelekea Petro na Yohana; ambao waliposhuka, wakawaombea wampokee Roho Mtakatifu; kwa maana bado hajawashukia hata mmoja wao, ila wamebatizwa tu kwa jina lake Bwana Yesu. Ndipo wakaweka mikono yao juu yao, nao wakampokea Roho Mtakatifu. Hata Simoni alipoona ya kuwa* <u>*watu wanapewa Roho Mtakatifu kwa kuwekewa mikono ya mitume*</u>*, akataka kuwapa fedha akisema, Nipeni na mimi uwezo huu, ili kila mtu nitakayemweka mikono yangu, apokee Roho Mtakatifu. Lakini Petro akamwamnbia, Fedha yako na ipotelee mbali pamoja nawe, kwa kuwa umedhania ya kuwa karama ya Mungu yapatikana kwa mali.*"

Matendo 8:6,12,14-20

18. Baada ya Filipo kuwekewa mikono na mitume alianza kuhubiri na kufanya ishara katika mji gani? _________________

19. Wakristo wa mji huo walipata Roho Mtakatifu kwa kuwekewa mikono ya nani? __________________

20. Ikiwa Filipo angaliweza kuwapa watu uwezo wa Roho Mtakatifu, je! mitume wangalikuwa na haja ya kusafiri mpaka Samaria na kuwawekea mikono? __________________

Baadhi ya watu husema kwamba haikuwa mitume tu walioweza kuwawekea watu mikono kusudi wafanye miujiza. Wanatukumbusha maneno ya Paulo jinsi alivyomwambia Timotheo:

"*Usiache kuitumia karama ile iliyomo ndani yako, uliyopewa kwa unabii na kwa kuwekewa mikono ya Wazee*." 1 Timotheo 4:14

Walakini imetupasa kukumbuka jinsi mtume Paulo naye aivyokuwa mmoja wapo wa wale waliomwekea Timotheo mikono. Maana Paulo aliendelea kumwambia akisema:

"*Kwasababu hiyo nakukumbusha, uichochee karama ya Mungu, iliyo ndani yako kwa kuwekewa mikono yangu.*" 2 Timotheo 1:6

21. Timotheo hakupewa uwezo wa Roho kwa kuwekewa mikono ya wazee tu bali kwa kuwekewa mikono ya mtume yupi? __________________

Mistari mingine ya Biblia inayothibitisha kwamba watu walipata uwezo wa Roho kwa kuwekewa mikono ya mitume ni Matendo 19:1-7 na maneno ya mtume Paulo kwa Wakristo wa Rumi katika Warumi 1:11.

## ROHO MTAKATIFU NA KORNELIO

Baadhi ya watu hutukumbusha jinsi mtu aitwaye Kornelio alivyopata uwezo wa Roho bila kuwekewa mikono ya mitume. Walakini, jambo hili halikuwa jambo la kawaida. La, bali mtume Petro mwenyewe alishituka kuliona. Wala watu leo wasidhanie kwamba wanaweza kupata Roho hivyo. Maana Kornelio alipewa Roho kwa sababu maalum. Kornelio hakuwa Myahudi bali alikuwa mtaifa. Torati ya Musa iliwakatalia Wayahudi wasiwe na ushirika na mataifa. Kwa hiyo, mitume wasingaliwawekea mikono wala kuwahubiria neno la Yesu. Basi, Mungu alimpa Petro ishara mbili kumwonesha kwamba mataifa wanaweza kubatizwa na kuokolewa. Kwanza, Petro alipewa maono (Matendo 10:11-20). Kisha, Kornelio na wenzake walianza kunena kwa lugha. Petro alipoyaona, mambo hayo alisema:

"*Ni nani awezaye kukataza maji, hawa wasibatizwe, watu waliopokea Roho Mtakatifu vile vile kama sisi? Akaamuru wabatizwe kwa Jina lake Yesu Kristo.*" Matendo 10:47-48

"*Na Petro alipopanda kwenda Yerusalemu, wale walio wa tohara (yaani, Wayahudi) wakashindana naye, wakisema, uliingia kwa watu wasiotahiriwa ukala nao. Petro akaanza kuwaeleza kwa taratibu, akasema… Ikawa nilipoanza kunena, Roho Mtakatifu akawashukia kama alivyotushukia sisi mwanzo. Nikalikumbuka neno lile la Bwana, jinsi alivyosema, Yohana alibatiza kwa maji kweli, bali ninyi mtabatizwa kwa Roho Mtakatifu. Basi ikiwa Mwenyezi Mungu amewapa wao karama ile ile aliyotupa sisi tuliomwamini Bwana Yesu Kristo, mimi ni nani niweze kumpinga Mungu? Waliposikia maneno haya wakanyamaza, wakamtukuza Mungu, wakisema, Basi, Mungu amewajalia hata mataifa nao toba liletalo uzima.*"

Matendo 11:2-4,15-18

22. Kornelio alipewa uwezo wa kunena kwa lugha ili iwe ishara kwa nani? __________________

23. Je! Petro angaliwapokea na kuwabatiza mataifa ikiwa asingalipewa ishara na Mungu? __________________

## MAANDIKO YANASEMA MIUJIZA ITAKOMA

Mtume Paulo aliongea kwa kirefu kuhusu ishara na miujiza katika 1Wakorintho milango ya 12 hadi 14. Baadhi ya mambo aliyoeleza ni haya yafuatayo:

"*Nijaposema kwa lugha za wanadamu na za malaika, kama sina upendo, nimekuwa shaba iliayo na upatu uvumao. Tena nijapokuwa na unabii, na kujua siri zote na maarifa yote, nijapokuwa na imani timilifu kiasi cha kuweza kuhamisha milima, kama sina upendo, si kitu mimi… Upendo haupungui neno wakati wo wote; bali ukiwapo unabii utabatilika; zikiwapo lugha, zitakoma; yakiwapo maarifa, yatabatilika… Basi, sasa inadumu imani, tumnaini, upendo, haya matatu; na katika hayo lililo kuu ni upendo.*"

1 Wakorintho 13:1-2,8,13

24. Mtume alisema unabii utafanyanini? __________________

25. Maandiko yanasema lugha zitafanya nini? __________________

26. Taja mambo matatu yanayodumu kuliko miujiza. __________________ na __________________ na __________________

Watu fulani hudhani kwamba karana za Roho zitaendelea mpaka Yesu atakapokuja tena. Walakini imetupasa kukumbuka jinsi Paulo alivyosema kwamba imani, na tumaini zitadumu kuliko miujiza. Kwa hiyo, ni lazima kwamba miujiza itakwisha <u>kabla hajaja Yesu</u>. Maana, atakapokuja Yesu, imani yetu itakwisha kwa sababu tukimwona yeye hatutabaki tena kuamini. Kuamini ni kusadiki kitu bila kukiona (2 Wakorintho 5:7; Waebrania 11:1). Vivyo hivyo, tumaini letu nalo litakoma atakapokuja Yesu, maana tutakuwa tumekwisha kufanyikiwa (Warumi 8:24). Basi, kwa sababu Biblia inasema kwamba imani na tumaini hudumu kuliko miujiza, ni Dhahiri kwamba miujiza itakuwa imekoma kabla hajaja Yesu.

27. Je! miujiza itadumu mpaka atakapokuja Yesu? __________________

## MIUJIZA ILIKOMA LINI?

Katika Yohana 16:13, Yesu aliwaahidi mitume kwamba watapewa Roho Mtakatifu ambaye atawaongoza na kuwatia kwenye kweli yote. Mitume walihubiri na kuyaandika katika vitabu mambo yale waliyofundishwa na Roho. Walakini, katika mwanzo wa kanisa, Wakristo hawakuweza kuvisoma vitabu vya Agano Jipya kusudi wajifunze mapenzi ya Mungu. Maana, mitume walikuwa bado hawajamaliza kuviandika. Kwa hiyo, Mungu aliwawezesha mitume kuwawekea mikono baadhi ya Wakristo wenzao kusudi wawepo manabii walioweza kufundisha katika mahali pasipokuwa na mitume (Warumi 1:11). Miujiza na ishara walizozifanya manabii ziliwaonyesha watu kwamba maneno yao yalitoka kwa Mungu

(Marko 16:20). Walakini, Mungu alikuwa akiwafunulia manabii maneno yake kwa sehemu tu wala si kwa ukamilifu. Ndiyo maana walitakiwa wawe wengi. Mtume Paulo alisema:

"*Na manabii wanene wawili, au watatu, na wengine wapambanue. Lakini mwingine aliyeketi akifunuliwa, neno, yule wakwanza na anyamaze. Kwa maana ninyi nyote mwaweza kuhutubu mmoja mmoja, ili wote wapate kujifunza, na wote wafarijiwe.*" 1 Wakorintho 14:29-31

"*Bali ukiwapo unabii utabatilika; zikiwapo lugha, zitakoma; yakiwapo maarifa, yatabatilika. Kwa maana tunafahamu kwa sehemu, na tunafanya unabii kwa sehemu; lakini ijapo ile iliyo kamili, iliyo kwa sehemu itabatilika.*" 1 Wakorintho 13:8-10

28. Mtume alisema kwamba manabii walifahamu na kufanya unabii kwa sehemu tu. Tena alisema kwamba ijapo ile iliyo kamili, iliyo kwa sehemu itafanya nini? _________________

Je! ni nini iliyo kamilifu? Bila shaka ni ufunuo kamili wa mapenzi ya Mungu jinsi ulivyo andikwa na mitume na manabii katika vitabu vya Agano Jipya. Maana, twasoma:

"*Unabii haukuletwa po pote kwa mapenzi ya mwanadamu; bali wanadamu walinena yaliyotoka kwa Mungu, wakiongozwa na Roho Mtakatifu.*" 2 Petro 1:21

"*Kila andiko, lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki; ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema.*" 2 Timotheo 3:16-17

29. Je! maandiko ya Biblia yatosha kumkamilisha mtu wa Mungu? _________________

30. Kwa kuwa maandiko yanatukamilisha katika kila tendo jema, je! tunazihitaji ishara leo? _________________

Mtume Paulo alisema kwamba unabii, lugha, na ishara zitakoma wakati ile iliyo kamili itakapofika. Basi, iliyo kamili imekwisha kufika. Kama tulivyoona huko juu, iliyo kamili ni sheria ya Yesu jinsi inavyofunuliwa kwa ukamilifu katika vitabu vya Agano Jipya. Kwa hiyo, hatuhitaji manabii na ishara leo. Maana mitume wameimaliza kazi ya kuifunulia kweli yote na kuiandika katika vitabu (Yohana 16:13; Wagalatia 1:8; Yuda 1:3; Yakobo 1:21-25). Wala haitoshi, bali uwezo wa kufanywa miujiza ulipatikana kwa kuwekewa mikono ya mitume ambao wote wamekufa. Kwa hiyo, hakuna mtu anayewezeshwa na Mungu kufanya ishara leo.

## MIUJIZA YA KISASA

Tangu siku za mitume wamekuwapo watu wanaowadanganya Wakristo. Yesu ametuonya kuhusu watu hawa akisema:

"*Watatokea makristo wa uongo, na manabii wa uongo, nao watatoa ishara kubwa na maajabu; wapate kuwapoteza, kama yamkini, hata walio wateule. Tazama, nimekwisha kuwaonya mbele.*" Mathayo 24:24-25

31. Je! watu wote wanaotoa ishara na maajabu wametoka kwa Mungu? _________________

Watu wengine hudhani kwamba mtu ye yote anayemtaja Yesu anapofanya mambo ya ajabu ametoka kwa Mungu. Lakini; wazo hili si kweli, maana Yesu alisema:

"*Wengi wataniambia siku ile, Bwana, Bwana, hatukufanya unabii kwa jina lako, na kwa jina lako kutoa pepo, na kwạ jina lako kufanywa miujiza mingi? Ndipo nitawaambia dhahiri, Sikuwajua ninyi kamwe; ondokeni kwangu, ninyi mtendao maovu.*" Mathayo 7:22-23

32. Je! watu wote wanaomtaja Yesu wanapofanya maajabu watakubaliwa naye? ________________

Paulo ametuonya kwamba Shetani anaweza kuwadanganya watu kwa ishara na maajabu, akisema:

"*Yule ambaye kuja kwake ni kwa mfano wa kutenda kwake Shetani, kwa uwezo wote, na ishara na ajabu za uongo; na katika madanganyo yote ya udhalimu kwa hao wanaopotea; kwa sababu hawakukubali kuipenda ile kweli, wapate kuokolewa.*" 2 Wathesalonike 2:9-10

"*Maana watu kama hao ni mitume wa uongo, watendao kazi kwa hila, wanaojigeuza wawe mfano wa mitume wa Kristo. Wala si ajabu. Maana Shetani mwenyewe hujigeuza awe mfano wa malaika wa nuru. Basi si neno kubwa watumishi wake nao wakijigeuza wawe mfano wa watumishi wa haki, ambao mwisho wao utakuwa sawasawa na kazi zao.*" 2 Wakorintho 11:13-15

33. Je! Shetani anaweza kujigeuza awe mfano wa Mkristo na kuwadanganya watu kwa ishara? ________________

Yesu alituambia jinsi tunavyoweza kuwatambua manabii na waalimu wa uongo. Alisema:

"*Jihadharini na manabii wa uongo, watu wanaowajia wamevaa mavazi ya kondoo, walakini kwa ndani ni mbwamwitu wakali… Ndiposa kwa matunda yao mtawatamnbua. Si kila mtu aniambiaye, Bwana, Bwana, atakayeingia katika ufalme wa mbinguni; bali ni yeye afanyaye mapenzi ya Baba yangu aliye mbinguni.*" Mathayo 7:15,20-21

34. Mtu asiyeyashika maneno yote ya Mungu ni nabii gani? ________________

Wako watu leo wanaosema kwamba wanao uwezo wa Roho Mtakatifu wa kutoa unabii, kunena kwa lugha, na kadhalika. Walakini, ukiyachunguza matendo yao na mafundisho yao utaona kwamba hawana Roho wa Mungu, maana wanamwasi Mungu. Kwa mfano, ikiwa ni Mungu ambaye anawawezesha kufanya ishara, basi bila shaka imewapasa kuyashika asharti aliyowapa mitume. Twasoma:

"*Kama mtu akinena kwa lugha, wanene wawili au watatu, si zaidi, <u>tena zamu kwa zamu</u>, na mmoja na afasiri. Lakini asipokuwapo mwenye kufasiri na anyamaze katika kanisa; aseme na nafsi yake tena, na Mungu. Na manabii wanene wawili, au watatu, na wengine wapambanue. Lakini mwingine aliyeketi akifunuliwa neno, yule wa kwanza na anyamaze. <u>Kwa maana ninyi nyote mwaweza kuhutubu mmoja mmoja, ili wote wapate kujifunza, na wote wafarijiwe</u>. Na roho za manabii huwatii manabii. Kwa maana Mungu si Mungu wa machafuko, bali wa amani; vile vile kama, ilivyo katika makanisa yote ya watakatifu. Wanawake na wanyamaze katika kanisa, maana hawana ruhusa kunena; bali watii, kama vile inenavyo torati nayo. Nao wakitaka kujifunza neno lo lote, na wawaulize waume zao wenyewe nyumbani mwao; maana ni aibu wanawake kunena katika Kanisa… Mtu akijiona kuwa ni nabii au mtu wa rohoni, na ayatambue hayo ninayowaandikia, ya kwamba ni maagizo ya Bwana.*" 1 Wakorintho 14:27-35, 37

35. Katika kanisa Mungu alisema kwamba manabii na watu wanenao kwa lugha wanene zamu kwa zamu. Tena, wasizidi wangapi? ________________

36. Je! Mungu aliwaruhusu wanawake kunena, au kutoe unabii au kuhubiri katika kanisa? ________________

37. Je! mtu ambaye anavunja amri hizo za Mungu hufanya ishara zake kwa nguvu ya Mungu au ya Shetani? ________________

Tena, mara nyingi watu wanaoamini kwamba Wakristo wanaweza kufanya ishara leo huasi amri ya Yesu ya kubatizwa katika maji. Watu hawa husema kwamba eti, watu wengi wamepata Roho Mtakatifu bila kubatizwa na, kwa hiyo, wanaweza kuokolewa bila kubatizwa katika maji. Wazo hili si kweli. Maana hata Kayafa, yule Kuhani Mkuu aliyemsulibisha Yesu, aliwahi kutabiri kwa nguvu ya Roho (Yohana 11:49-53). Lakini Kayafa hakuokolewa hata ingawa alikuwa na Roho. Tena, hata ingawa Kornelio alipewa Roho kabla hajabatizwa, lakini alikuwa hajaokolewa bado. Maana, Yesu alisema:

"*Amin, amin, nakuambia, Mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho, hawezi kuuingia ufalme wa Mungu.*"
Yohana 3:5

Kwahiyo, Petro alimwamuru Kornelio kubatizwa katika maji (Matendo 10:47-48). Soma pia Marko 16:16 na Matendo 2:38. Sauli naye hakuokolewa kwa kumwona Yesu wala kwa kuponyeshwa macho kwa nguvu ya Roho, bali aliambiwa:

"*Basi sasa unakawilia nini? Simama, <u>ubatizwe, ukaoshe dhambi zako</u>, ukiliitia jina lake.*" Matendo 22:16

38. Watu hawaokolewi kwa kupewa Roho, bali Yesu alisema kwamba ni lazima kuzaliwa tena kwa Roho na kwa nini pia? ________________

39. Je! mtu anayesema kwamba watu wanaweza kuokolewa bila kubatizwa katika maji ana Roho wa Mungu au roho wa Shetani? ________________

## ONYO

Maneno ya Biblia yatosha kumkamilisha Mkristo bila kuona ishara. Yesu alituonya kwa njia ya mfano akieleza habari ya mtu mwovu aliyekufa. Huko kuzimu, yule mwovu alipokuwa katika mateso, akaanza kuwakumbuka ndugu zake ambao hawajafa bado. Akainua macho yake akamwona Ibrahimu pamoja na Lazaro, mtu mwema aliyekufa. Basi akamwomba Ibrahimu amtume Lazaro duniani awaonye wale ndugu zake. Walakini Ibrahimu alikataa akisema:

"*Wanao Musa na manabii, na wawasikilize wao. Akasema, La, baba Ibrahimu, lakini kama akiwaendea mtu atokaye kwa wafu, watatubu. Aka mwambia, Wasipowasikia Musa na manabii, hawatashawishwa hata mtu akifufuka katika wafu.*" Luka 16:29-31

Vivyo hivyo, sisi tusipomwamini Yesu kwa sababu ya maneno yaliyoandikwa katika Biblia basi, tusingemwamini hata tungeona ishara. Katika Injili ya Yohana twasoma:

"*Basi kuna ishara nyingine nyingi alizozifany a Yesu mbele ya wanafunzi wake, zisizoandikwa katika kitabu hiki. Lakini hizi zimeandikwa; ili mpate kuamini ya kwamba Yesu ndiye Kristo, Mwana wa Mungu; na kwa kuamini mwe na uzima kwa jina lake.*" Yohana 20:30-31

40. Mtu asiyemwamini Yesu kwa sababu ya yale yaliyoandikwa katika Biblia, je! angeamini kama angeona ishara? _________________

Imewapasa watu ambao hutaka kuona miujiza leo kukumbuka maneno ya Yesu yafuatayo:

"*Baadhi ya waandishi na Mafarisayo wakamjibu, wakasema, Mwalimu, twataka kuona ishara kwako. Akajibu, akawaambia, Kizazi kibaya na cha zinaa chatafuta ishara.*" Mathayo 12:38-39

*************************************************************************************

Jina lako ………………………………………………
Anwani yako ……………………………………………

***KANISA la KRISTO***

***Tanzania***